

KWA: Mzazi/Mlezi wa Mtoto wa Chekechea

KUTOKA: Mpango wa Upimaji wa Lazima wa Kiwango wa Sumu ya Risasi kwenye Damu
(Mandatory Blood Lead Testing Program)

**MADA: Mtoto wako huenda anahitaji kupimwa kiwango cha
sumu ya risasi kwenye damu**

Kulingana na rekodi za Idara ya Iowa ya Afya na Huduma za Binadamu (Iowa Department of Health and Human Services), mtoto wako wa chekechea huenda hakufanyiwa kipimo cha kiwango cha sumu ya risasi kwenye damu. Ikiwa mtoto wako amefanyiwa kipimo cha kiwango cha sumu ya risasi kwenye damu katika umri wowote kabla ya kufikisha miaka 6, tafadhali puuza barua hii.

Ikiwa mtoto wako hajapimwa, mpeleke akafanyiwe kipimo cha kiwango cha sumu ya risasi kwenye damu haraka iwezekanavyo. Bima za Medicaid, Hawk-i na mipango mingi ya bima hulipia kipimo cha kiwango sumu ya risasi kwenye damu. Ikiwa hauna namna ya kulipia kipimo hiki na mtoto wako ana umri wa miaka 5 au chini, wasiliana na idara yetu au shirika la afya ya umma karibu nawe ili usaidiwe kupata mahali ambapo mtoto wako anaweza kupimwa kiwango cha sumu ya risasi kwenye damu.

Visa vya sumu ya risasi hutokea kwa watoto katika Iowa. Hatua ya kupimwa kiwango cha sumu ya risasi kwenye damu ndio njia pekee ya kujua ikiwa mtoto wako ana sumu hii ya risasi.

In 2008, Jimbo la Iowa liliidhinisha sheria ya Upimaji wa Lazima wa Kiwango cha Sumu ya Risasi kwenye Damu (Mandatory Blood Lead Testing) inayohitaji watoto wote wanaojiunga na chekechea wapimwe angalau mara moja kwa kiwango cha sumu ya risasi kwenye damu.

Ikiwa una maswali na/au wasiwasi, tafadhali wasiliana na mpango:

Iowa Department of Health and Human Services
Lead Poisoning Prevention Program
321 E. 12th Street
Des Moines, IA 50319
Simu: 1-800-972-2026 Faksi: (515) 281-4529